Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لَا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 81 No. 227 | SAFAR - JAM.I 1443 AH | OKT - DIS 2021 | TAB.-FAT 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Na Hatuwatumi Mitume ila wawe watoaji wa habari njema na waonyaji. Na wale waliokufuru wanajadili kwa uwongo ili kwayo waibatilishe haki; na wakazifanya Aya Zangu na yale waliyoonywa kuwa mzaha. (Al Kahf: 18:57)

Afghanistani na chanzo cha kujikwaa



Mbegu ya matatizo katika nchi nyingi ilipandwa juzi na mavunondiyohayotunayovuna leo. Ni jana tu inayoweza kukueleza leo. Mwandishi Rajabu Mkieti kafafanua yanayoendelea Afghanistan na nini cha kufanya ili nchi hii itengemae...

Wanamgambo wa kundi la talibani wamerudi tena kuiongoza ikulu ya Kabul nchini Afghanistan baada ya miaka 20 ya vita...

Makala uk. 2

Maisha ya Mtume Mtukufu Muhammad saw

Yalivyosimuliwa na Hadhrat Mirza Bashir ud Din Mahmud Ahmad r.a. Khalifatul Masih wa pili wa Masihi Aliyeahidiwa as

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

BISHARA YA USHINDI WA WARUMI

Ndani ya siku hizo hizo kukatokea vita ya hatari kati ya Kisra na Kaisari na Kisra akashinda. Majeshi ya Kiirani yakasambaa hadi Sham (Syria). Yerusalem ikaangamizwa kiasi ya kwamba jeshi la Wairan likafika hadi Ugiriki na Asia ya Kochak na wakasimika hema yao mbele ya Bass Force iliyokuwa maili kumi tu kutoka Constantinia. Watu wa Makka wakaifurahia fursa hii na wakasema kwamba uamuzi wa Mwenyezi Mungu umedhihirika. Waabudu masanamu wa Kiirani wamewashinda Wakristo walio watu wa Kitabu. Wakati huo (Mtume saw) akafahamishwa na Mwenyezi Mungu kwamba:

غُلِبَتِ الرُّوْمُ ۙ﴿۳﴾
فِيْٓ اَدْنَى الْاَرْضِ وَهُمْ مِّنْۢ بَعْدِ غَلَبِهِمْ
سَيَغْلِبُوْنَ ۙ﴿۴﴾
فِيْ بِضْعِ سِنِيْنَ ؕ لِلّٰهِ الْاَمْرُ مِنْ قَبْلُ وَمِنْۢ
بَعْدُ ؕ وَيَوْمَئِذٍ يَّفْرَحُ الْمُؤْمِنُوْنَ ۙ﴿۵﴾
بِنَصْرِ اللّٰهِ ؕ يَنْصُرُ مَنْ يَّشَآءُ ؕ وَهُوَ الْعَزِيْزُ
الرَّحِيْمُ ۙ﴿۶﴾
وَعْدَ اللّٰهِ ؕ لَا يُخْلِفُ اللّٰهُ وَعْدَهٗ وَلٰكِنَّ
اَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿۷﴾

Yaani *jeshi la Warumi limeshindwa karibuni na nchi za Waarabu, lakini litashinda tena baada ya kushindwa kwake ndani ya miaka michache. Kanuni ya Mwenyezi Mungu itaendelea kama ilivyokuwa hapo awali. Itakapofika siku hiyo ya ushindi, waaminio pia, katika wakati huo, watapata furaha ya msaada wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu Humsaidia Amchaguaye. Yeye ni mwenye shani kubwa na ni Mwingi wa Ukarimu. Hiyo ni ahadi ya Yule Mungu Asiyebadilisha ahadi Yake. Lakini watu wengi hawazijui kudra za Mwenyezi Mungu.*

Miaka michache tu baadae, Mwenyezi Mungu Akaitimiza bishara hii. Upande mmoja Warumi wakaiokoa nchi yao baada ya kuwashinda Wairani, na upande wa pili, kama ilivyosemwa, ndani ya siku hizo hizo, Waislamu wakaanza kupata ushindi dhidi ya watu wa Makka, wakati watu wa Makka walikuwa wakidhani hivi kwamba wao wameshaimaliza Islam baada



ya kuwakataza watu kusikiliza habari za Islam na kuwahamasisha kuwafanyia dhulma Waislamu. Maneno ya Mwenyezi Mungu yaliendelea mfululizo kutoa habari za ushindi wa Islamu kwamba saa ya kuangamia kwa watu wa Makka inakaribia.

Hivyo ndani ya siku hizo hizo Mtume Muhammad s.a.w. akautangaza kwa nguvu sana Wahyi huu wa Mwenyezi Mungu usemao:

وَقَالُوْا لَوْلَا يَاْتِيْنَا بِاٰيَةٍ مِّنْ رَّبِّهٖ ؕ اَوَلَمْ
تَاْتِهِمْ بَيِّنَةُ مَا فِي الصُّحُفِ الْاُوْلٰى ﴿۱۳۴﴾
وَلَوْ اَنَّآ اَهْلَكْنٰهُمْ بِعَذَابٍ مِّنْ قَبْلِهٖ
لَقَالُوْا رَبَّنَا لَوْ لَآ اَرْسَلْتَ اِلَيْنَا رَسُوْلًا
فَنَتَّبِعَ اٰيٰتِكَ مِنْ قَبْلِ اَنْ نَّذِلَّ
وَنَخْزٰى ﴿۱۳۵﴾
قُلْ كُلٌّ مُّتَرَبِّصٌ فَتَرَبَّصُوْا ۚ
فَسَتَعْلَمُوْنَ مَنْ اَصْحٰبُ الصِّرَاطِ
السَّوِيِّ وَمَنِ اهْتَدٰى ﴿۱۳۶﴾ ع ۱۷

Yaani *watu wa Makka wanasema kwamba kwa nini Muhammad*

Endelea uk. 3

Ufahamu mpango wa Waqf-e-Jadid uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

SI MADOGO HAYO!!

Ukamilifu wa Mwislamu ni kutomchukua yeyote kuwa kigezo chake isipokuwa Mtukfu Mtume Muhammad s.a.w. Tunafanya makossa makubwa kufikiri kuwa hili jambo ni dogo na hili ni kubwa. Busara ni kutekeleza yote aliyoagiza mbora wa viumbe wote na kuachana na vyote alivyokataza na hiyo ndiyo nusura yetu.

Tunafundishwa ya kwamba ni lazima kuanza kazi zetu kwa Bismillah. Kwa kufanya hivyo tunajiongezea Baraka na kupata msaada wa Allah kwa hayo tunayofanya. Inawezekana tukasahau na ndio maana tunakumbushana.

Kwa sababu ya kutapakaa kwa umagharibi na mbwembwe hizo za haki za binadamu ili uonekane mtu wa kisasa basi unapeana mikono na akina mama, wengine wanakwenda mbali na kukumbatiana kwa mtu ambaye si tu humjui bali haijaruhusiwa katika Islam kufanya hayo unayoyafanya.

Hoja itajitokeza lakini mara nyingine unalazimika kupeana mikono na viongozi wakubwa au una shida fulani ukitafuta visingizio havikosi vipo chungu nzima. Lakini wanaomhofu Allah wameviondoa visingizio hivyo. Yupo sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa^{as} ambaye hakumpa mkono Malkia wa Uingereza na alipoulizwa akasema hayo ni mafundisho ya dini yake. Mbashiri Mkuu mmoja alikuwa anaandika kitabu *Mwana Mkuu wa Ibrahim*, alipofika Ubalozi wa Ujerumani mama aliyetakiwa kumpa karatasi aliyokuwa anahitaji alikuja kwanza kumsalimu kwa kutoa mkono, bila kujali hatua hiyo ingemfanya asitoe karatasi au atoe. Kati ya karatasi na mafundisho ya dini yake alichagua dini yake. Ni wangapi kati yetu hivi leo wanaweza kuwa na ujasiri huo?

Kuna umagharibi mwingine unaowasumbua watu kutumia mkono wa kushoto. Mafundisho yako bayana katika Islam ya kwamba tunatumia mkono wa kushoto mahali panapohusika. Vingine mkono wa kulia ndio umepewa kipaumbele. Wa kulia na wa kulia wako. Ukiingia mahotelini utamuona kijana au binti wa Kiislam akitumia mkono wa kushoto, ni kosa. Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alipokuwa anakunywa maji alitumia mkono wa kulia, kula mkono wa kulia, wakati wa kutawadha, wakati wa kuoga, kipaumbele ni mkono wa kulia.

Kuran Tukufu ni mwongozo kwa waaminio. Ni maagizo na sharia sio za kusikiliza tu bali kutekeleza. Hivyo inasomwa lazima uache shughuli zote, usikilize ili upate kurehemewa. Ni wangapi tunatulia na kusikiliza Kurani Tukufu inaposomwa? Kusikiliza ni njia mojawapo ya kurehemewa. Kwa nini tufunge mlango huu wa neema wa kutosikiliza Kurani Tukufu inaposomwa?

Upo pia udhaifu, mimi hili hapana shaka nitalifanya kesho. Hili naliweza kabisa, wasiwasi gani kesho nitakuja! Kumbuka sana wewe ni binadamu, tena dhaifu, dhaifu sana. Ya kesho unayajuaje? Hata ya sekunde inayofuata unajigamba nayo vipi? Wewe hakuna ulilo nalo bila ya uwezo na mapenzi ya Allah. Tujenge utamaduni wa kutumia neno InshaAllah. Hiyo ni kukiri udhaifu wetu. Hiyo ni kukiri kuwa hakuna tunachoweza. Hiyo ni kuomba msaada. Ni kuomba hifadhi. Tukumbuke neno InshaAllah. Kwa kufanya hivyo tunakabidhi kila kitu mikononi mwa Allah na ukishamkabidhi Yeye ndiye Anayefanya anavyotaka. Ni mapenzi Yake peke yake yanaweza kukunusuru katika dunia hii iliyojaa miba kwa kila hatua unayopiga.



Afghanistani na chanzo cha kujikwaa

Rajabu Mkieti
Ikwiriri, Rufiji

Tayari wanamgambo wa kundi la Talibani wamerudi tena kuiongoza ikulu ya Kabul nchini Afghanistani. Hii ni baada ya miaka 20 ya vita iliyopigwana kati ya Marekani na kundi la wanamgambo wa Talibani. Vita iliyogharimu maisha ya maelfu ya askari, raia, rasilimali fedha na vifaa vya kijeshi pamoja na uharibifu mkubwa wa mazingira. Kundi la wanamgambo wa Talibani lilifurushwa na vikosi vya Marekani na washirika wake na kutangazwa kuwa kundi la Talibani ni magaidi. Inakadiriwa kuwa watu 160,000 wamepoteza maisha. Kwa mujibu wa Idara ya Ulinzi ya Marekani, kutoka Oktoba 2001 hadi Septemba 2019, taifa hilo lilikuwa limetumia wastani wa dola 800 bilioni kwa ajili ya kazi za kijeshi.

Kinachoendelea hivi sasa nchini humo ni zama mpya za utawala wa dola inayoongozwa kwa kufuata nidhamu ya serikali ya Kiislam. Hii imetokea baada ya wanamgambo hao wa Talibani kuiteka ikulu ya Kabul na kuuondoa utawala uliowekwa kwa mwavuli wa mataifa ya magharibi baada ya Marekani kuondoa vikosi vyao. Kuondoka kwa vikosi hivyo kumekamilisha ahadi ya Rais Joe Biden wa Marekani aliyeahidi kumaliza vita hivyo kwa kuondoa vikosi vya jeshi kutoka Kabul mpaka kufikia Agosti 30 2021, akisimamia pia makubaliano yaliyofikiwa na watangulizi wake.

Oktoba 7, 2001 ndio siku Marekani ilipoivamia Afghanistani iliyokuwa chini ya Talibani na kuanza mashambulizi kwa lengo la kuwaangamiza wanamgambo wa Talibani na Kundi la Al-Qaeda.

Kuanzia Oktoba 7, 2001 mpaka Agosti 30 2021, ni miaka 20, iliyojaaa damu, hofu, mashaka na udhalilishaji mkubwa wa haki za binadamu. Hakuna aliyetarajia ukubwa wa mashambulizi yaliyoanza siku hiyo, ingawa vita hii imetokea baada ya majengo mawili makubwa ya kibiashara ya Marekani kushambuliwa na kundi la Al –Qaida Septemba 11, 2001. Baada ya shambulio la Septemba 11, 2001 Marekani na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa liliitaka Taliban waliokuwa wanashikilia sehemu kubwa ya Afghanistan tangu mwaka 1996 kumsalimisha Osama bin Laden kiongozi wa Al-Qaida kwa ajili ya kufunguliwa mashtaka ya uhalifu. Mamlaka ya serikali ya Kabul ilikataa kumsalimisa Osama kwa Marekani. Marekani ikafanya uamuzi na kuivamia ghafla Afghanistani Oktoba 7, 2001 kwa kushambulia kwa makombora makao ya Taliban na Al-Qaeda kwenye miji ya Kabul, Kandahar, Jalalabad, Kunduz na Mazar-e-Sharif.

Rais wa wakati huo George Bush wa Marekani alijitokeza hadharani na kutangaza kwamba Marekani inapigana vita dhidi ya ugaidi. Tangazo hilo lilifutilia mbali hadhi na heshima ya Talibani katika dunia juu ya utawala wa uadilifu wa nidhamu ya mfumo wa uongozi wa kiislamu, kundi hilo lililokuwa likiiongoza Afghanistani.

Makubaliano ya mkataba baina kundi la Talibani na Marekani yaliyotiwa saini mjini Doha, Qatar February 29, 2020 yanaipa tena hadhi ya kundi la Talibani kuendelea kufanya shughuli zao za kisiasa na kiutawala.

Mkataba wa mjini Doha unaipa nguvu Talibani juu ya kulinda amani ya Afghanistani na kufichua magaidi katika nchi hiyo. Bado kuna kasoro kadhaa zinazotokea katika utawala wa Talibani juu ya kusimamia serikali ya Aghanistani hususan matumizi ya misimamo mikali ya kuiongoza serikali na mtazamo wao juu ya Jihadi katika serikali yao. Mambo hayo yanatoa mwanya wa wazi kwa watu wasiokuwa Waislamu kuilaumu dini tukufu ya Islamu kuwa ndio inayofundisha misimamo mikali, jihadi ya kujitoa mhanga na kutoangalia haki za wengine hususan haki za wanawake na watoto katika nchi. Kiukweli kabisa serikali nyingi zinazotawala kwa jina la Islamu, si Uislamu bali zipo mbali sana na dhana ya serikali ya mfumo wa Kiislamu. kinachoendelea hivi sasa kwa nchi ya Afghanistani na nchi nyinginezo zinazotawaliwa na dhana ya serikali ya mfumo wa Kiislamu si Uislamu bali ni taamaa ya madaraka na pupa za kutaka mali na mapenzi ya dunia, kuminya haki za wanawake, kwa vazi la dini ya tukufu ya Islamu. Hii hatuwezi kuiita serikali ya Kiislamu katu bali itakuwa ni kuivisha dini tukufu ya Islamu kilemba cha ukoka. Na kwa hakika ni jambo la aibu kudai serikali ya Afghanistani, Irani, Pakistani au nyinginezo kuwa ni serikali za mfumo wa Kiislamu. Kama wachunguzi wa maswala ya kisiasa katika nchi za magharibi watajitia chongo kwa kutochunguza sawa sawa kwa uangalifu na ufasaha na makini mno mfumo wa serikali hizo nilizozitaja hapo juu na waendelee kutoa maoni yao kuwa serikali hizo ni za Kiislamu na zinafuata mfumo sahihi wa Islamu, basi na sisi tunayo haki kudai kuwa mapinduzi ya Kiingereza yalitokea 1640-1689 (*The English Revolution*, 1640-1689), machafuko ya Ukreini na Cuba kuwa ni mapinduzi yaliyoendeshwa kwa baraka za dini ya Kikristo. Ikiwa mifano hiyo niliyoitaja sio sahihi katika nchi zinazoongozwa

Endelea uk. 4

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Maisha ya Mtume Muhammad *saw*



Kutoka uk. 1

hatuletei ishara kutoka kwa Mola Wake. Je zile bishara za manabii waliopita zinazomsadikisha sio ishara zinazowatosha? Kama Sisi Tungewaangamiza watu wa Makka kabla ya kuwahubiria basi watu wa Makka wangeweza kusema kwamba Ewe Mola wetu, mbona hukutuletea Mtume yeyote? Tungeweza kuyafuata mafundisho Yako kabla hatujadhalilika. Waambie kwamba kila mtu anapaswa kuusubiri wakati wake. Hivyo nanyi pia isubirini saa ile wakati ambapo dalili itakapotimia ndipo kwa yakini mtakapofahamu kwamba ni nani anyetembea juu ya njia iliyonyooka na juu ya mwongozo wa Mwenyezi Mungu. (Twaha 134-136) Kila siku Wahyi mpya wa Mwenyezi Mungu ulikuwa ukiteremka na kila siku (Wahyi huo) ulikuwa ukitoa habari ya maendeleo ya Islam na ya maangamio ya Makafiri. Upande mmoja watu wa Makka walikuwa wakiitazama shani na nguvu yao na upande wa pili walikuwa wakiutazama udhaifu wa Muhammad saw na wa wenzake. Na halafu wakawa wakisoma ndani ya funuo za Mtume s.a.w. habari za misaada ya Mwenyezi Mungu na habari za mafanikio ya Waislamu, hivyo wakawa wanastaajabu na kudhani kwamba je wao wamekuwa wendawazimu au Muhammad s.a.w. ndiye amekuwa mwehu?

Watu wa Makka walikuwa na matumaini haya kwamba kutokana na dhulma na kupita kwetu kiasi dhidi ya Waislamu, sasa Waislamu walipaswa kuja upande wetu na hata Mtume s.a.w. mwenyewe pia na wafuasi wake pia walipaswa kuwa wameshikwa na shaka juu ya madai yake.

Na Mtume s.a.w. alikuwa akitoa tangazo hili kwamba

فَلَآ اُقۡسِمُ بِمَا تُبۡصِرُوۡنَ ﴿۳۹﴾

وَمَا لَا تُبۡصِرُوۡنَ ﴿۴۰﴾

اِنَّهٗ لَقَوۡلُ رَسُوۡلٍ كَرِيۡمٍ ﴿۴۱﴾

وَّ مَا هُوَ بِقَوۡلِ شَاعِرٍ ؕ قَلِيۡلًا مَّا تُؤۡمِنُوۡنَ ﴿۴۲﴾

اِنَّهٗ لَقَوۡلُ رَسُوۡلٍ كَرِيۡمٍ ﴿۴۱﴾

وَّ مَا هُوَ بِقَوۡلِ شَاعِرٍ ؕ قَلِيۡلًا مَّا تُؤۡمِنُوۡنَ ﴿۴۲﴾

وَلَا بِقَوۡلِ كَاهِنٍ ؕ قَلِيۡلًا مَّا تَذَكَّرُوۡنَ ﴿۴۳﴾

تَنۡزِيۡلٌ مِّنۡ رَّبِّ الۡعٰلَمِيۡنَ ﴿۴۴﴾

وَلَوۡ تَقَوَّلَ عَلَيۡنَا بَعۡضَ الۡاَقَاوِيۡلِ ﴿۴۵﴾

لَاَخَذۡنَا مِنۡهُ بِالۡيَمِيۡنِ ﴿۴۶﴾

ثُمَّ لَقَطَعۡنَا مِنۡهُ الۡوَتِيۡنَ ﴿۴۷﴾

فَمَا مِنۡكُمۡ مِّنۡ اَحَدٍ عَنۡهُ حٰجِزِيۡنَ ﴿۴۸﴾

وَ اِنَّهٗ لَتَذۡكِرَةٌ لِّلۡمُتَّقِيۡنَ ﴿۴۹﴾

وَ اِنَّا لَنَعۡلَمُ اَنَّ مِنۡكُمۡ مُّكَذِّبِيۡنَ ﴿۵۰﴾

وَ اِنَّهٗ لَحَسۡرَةٌ عَلَى الۡكٰفِرِيۡنَ ﴿۵۱﴾

وَ اِنَّهٗ لَحَقُّ الۡيَقِيۡنِ ﴿۵۲﴾

فَسَبِّحۡ بِاسۡمِ رَبِّكَ الۡعَظِيۡمِ ﴿۵۳﴾

Enyi watu wa Makka, hamko sahihi katika yale mnayoyadhania. Ninasema kwa kuapa, kwamba yale mambo muyaonayo na yale msiyoyaona, mnasikilizishwa Kurani hii kwa ulimi wa Mtume mwenye kuheshimika. Haya sio maneno ya mshairi. Bali mna imani kidogo tu mioyoni mwenu. Haya sio makisio ya mpiga ramli. Lakini yasikitisha kwamba ni nasaha ndogo tu mnazozipata. Hii imeteremshwa kutoka kwa Yule Aliyewaumba walimwengu wote, na Mimi Niliye Mola wa walimwengu wote Nakuambieni kwamba, kama yeye (Muhammad saw) angejitungia aya moja tu na kuinasibisha kwetu, basi Tungelimkamata kwa mkono wa kuume, kisha Tungeukata mshipa wake mkubwa wa damu. Na hata kama ninyi wote mngeungana na kutaka kumuokoa, msingeweza kumuokoa. Lakini Kurani hii ni nasaha kwa wale wenye kumuogopa Mwenyezi Mungu. Nasi Twafahamu kwamba miongoni mwenu wapo wenye kuikadhibisha Kurani hii. Lakini pia Twafahamu kwamba, mafundisho yake yanawakatisha tamaa wapinzani wake nao wanasema kwamba laiti tungekuwa na mafundisho haya. Nasi pia Twafahamu kwamba yale mambo yameyoelezwa ndani ya Kurani hii, yatatimia neno kwa neno. Hivyo Ewe Muhammad s.a.w., usiujali upinzani wa watu hawa na endelea kuueleza utakatifu wa jina la Mola Wako Mwenye shani.

Hatimae Haji ya tatu ikafika na misafara ya mahujaji wa Madina iliyojumuisha kundi kubwa la Waislamu ikawasili Makka. Kutokana na upinzani wa watu wa Makka, watu wa Madina wakataka kumuona Mtume s.a.w. faraghani. Sasa akili ya Muhammad saw ilikuwa tayari imeshaelekea upande huu kuwa huenda imekadiriwa kuhamia Madina. Aliwaambia mawazo yake ndugu na jamaa zake anaowaamini nao wakaanza kumshawishi (wakimwambia) usifanye hivyo, kwani ingawa watu wa Makka ni maadui, lakini hata hivyo miongoni mwao wamo ndugu na jamaa zako wenye athari. haieleweki Madina kutakuwaje. Ndugu zako wanaweza kukusaidia huko au la.

Lakini kwa kuwa yeye alishafahamu kwamba huu ndio uamuzi wa Mwenyezi Mungu, hivyo akakataa rai za ndugu na jamaa zake na akafanya uamuzi wa kwenda Madina. Ulipopita usiku wa manane, Mtume s.a.w. na Waislamu wa Madina wakakutana tena katika bonde la Uqba. Sasa pamoja naye, alikuwepo pia baba yake mdogo, Abbas r.a. Wakati huu idadi ya Waislamu wa Madina ilikuwa ni sabini na tatu. Miongoni mwao, sitini na mbili walikuwa ni wa kabila la Khazraj na kumi na moja walikuwa ni wa kabila la Aus. Na katika msafara huo walikuwemo pia wanawake wawili ambaye mmoja wao alikuwa ni mwanamke wa kabila la Banu Najjar aliyeitwa Ummi Ammaara.

Kwa kuwa maelezo ya Uislamu yalikuwa yameshawafikia watu hawa kwa kupitia Bwana Muswab, watu hawa walikuwa wamejaa imani na yakini. Matukio ya baadae yalidhihirisha kwamba watu hawa watathibitika baadae kuwa ni nguzo ya Islam. Ummi Ammara aliyejumuika siku hiyo, aliingiza upendo wa Islam ndani ya vizazi vyake kwa kiwango hiki kwamba, wakati mtoto wake aliposhikwa mateka na jeshi la Musailimah Kadhaab baada ya kifo cha Mtume s.a.w., basi Musailimah alimuitisha na kumuuliza kwamba je wewe washuhudia kuwa Muhammad saw ni Mtume wa Allah? Khubaib akasema; Naam. Kisha Musailimah akamuuliza; Je unashuhudia kuwa mimi ni Mtume wa Allah? Khubaib akasema Hapana. Hapo Musailimah akaamuru kwamba mkono wake mmoja ukatwe. Ndipo Musailimah akamuuliza tena kwamba je unashuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah? Khubaib akasema ndio. Kisha akamuuliza tena je unashuhudia kuwa mimi ni Mtume wa Allah? Khubaib akasema;Hapana. Kisha akaamuru akatwe kiungo chake kingine cha mwili. Na kila baada ya kumkata kiungo cha mwili alikuwa akimuuliza kwamba je unashuhudia kuwa mimi ni mtume wa Allah na Khubaib alikuwa akijibu; Hapana. Kwa namna hii viungo vyake vyote vya mwili vikakatwa. Na hatimae, akikatwa vipande vipande kwa njia hii, aliitangaza imani yake na kuiaga dunia.

Ummi Amara mwenyewe alishiriki katika vita nyingi pamoja na Mtume s.a.w. Kwa uchache hilo lilikuwa ni kundi lililokuwa na uaminifu na imani, ambao watu wake hawakuwa wamekuja kumuomba Mtume saw mali na utajiri, bali walikuja tu kuomba imani.

Abbas r.a. aliwaambia kwamba: Enyi watu wa kabila la Khazraj! Kipenzi chngu huyu ni mtu mwenye kuheshimika ndani ya kaumu yake. Watu wa kaumu yake humlinda wawe Waislamu au la. Lakini sasa yeye ameamua kuja kwenu. Enyi watu wa Khazraj! Kama yeye akija kwenu, basi Bara Arabu yote itakuwa dhidi yenu. Kama wataka kumchukua mkilifahamu jukumu lenu na kuzielewa hatari zile zitakazokujieni kutokana na kuihami dini yake, basi mchukueni kwa furaha, waila jiepusheni na dhamira hii.

Kiongozi wa msafara ule alikuwa ni Al Barraa. Alisema: Tumeyasikia maneno yako. Sisi tuko imara ndani ya dhamira yetu. Tumeyatoa mhanga maisha yetu kwa Nabii wa Mwenyezi Mungu. Sasa uamuzi ni wake, sisi tutaukubali kila uamuzi wake. Hapo Mtume s.a.w. akaanza kuwapa mafundisho ya Islam na akawapa mawaidha ya Umoja wa Mwenyezi Mungu na kuwaambia kwamba kama wao wanatoa ahadi ya kuilinda Islam kama wawalindavyo wake na watoto wao, basi yuko tayari kwenda nao. Alikuwa hajamaliza kuongea maneno yake ambapo watu sabini na mbili wa Madina, kwa kauli moja, wakaitikia ndio ndio. Walipandwa na jazba wakati huo kiasi ya kughafilika na utukutu wa watu wa Makka na sauti zao zikavuma angani.

Abbas akawatahadharisha akiwaambia keleleni, keleleni. Isije watu wa Makka wakalifahamu tukio hili. Lakini wakati huo walikuwa wameshaipata imani, sasa mauti kwao ilikuwa imeshakuwa ni jambo duni tu. Kiongozi wao mmoja alisema baada ya kusikia neno la Abbas r.a.: Ewe Mtume wa Allah! sisi hatuogopi. Wewe toa tu ruhusa sasa hivi tupigane vita na watu wa Makka tukiwa tayari kulipa kisasi cha dhulma waliyokutendea. Mtume s.a.w. akasema; Mwenyezi Mungu Hajanipa bado hukumu ya kusimama na kukabiliana nao. Baada ya hapo watu (hao) wa Madina wakafanya Baiat yake na kikao hicho kikaishia hapo.

Watu wa Makka wakapata taarifa ya tukio hili nao wakaenda kushitaki kwa viongozi wa Madina. Lakini kwa kuwa Abdullah bin Ubbay bin Salul alikuwa ndiye kiongozi wa msafara wa madina, hivyo hakuwa na taarifa kamili ya tukio hili. Yeye aliwatuliza na kuwaambia wao watakuwa tu wamesikia uvumi wa uongo, kwani hakuna tukio lolote la aina hii, kwani watu wa Madina huwa hawafanyi jambo lolote lile bila ya ushauri wangu. Lakini alikuwa hafahamu kwamba sasa ndani ya mioyo ya watu wa Madina ufalme wa Mungu ulikuwa umeshastawi badala ya ule wa Shetani. Baada ya hapo msafara wa Madina ukarejea.

KUHAMIA MADINA TOKA MAKKA

Itaendelea toleo Lijalo

Waqf-e-Jadid

Na **Sheikh Karimuddin Shams**

Kama tunavyofahamu kuwa mpango wa Tahrik e Jadid ni mpango mkuu wa shuguli nzima za mahubiri hivyo ndivyo Wakf e Jadid ni mpango ulio juu kabisa kuliko mipango yote yahusuyo malezi. Kama Tahrik e Jadidi ni jina la kuzishinda nchi kwa ajili ya Mungu na Mtume wake s.a.w. basi Wakfe Jadid ni kumlea vyema kila muahmadiyya wa nchi hizo, hivyo kwa ajili ya kuwapatia malezi mema wakazi wa vijijini.

Kuanzishwa kwa Wakfe Jadid

Hazrat Khalifa tul Masih wa Pili wa seyyedna Ahmad a.s. alitangaza mpango Fulani bila kuitaja Wakfe Jadid mnamo 9 Julai 1957 katika hotuba yake ya Idi ya Dhabihu na kusema: *"kwa ukweli Idi ya dhabihu inatuelekeza kwamba tutoke majumbani mwetu na kuenda poorini kwa ajili ya kutukuza jina la Mwenyezi Mungu pale na kuwasomesha watu kalima tukufu ya Mtume Wake kama walivyofanya Wasufi(Mawalii) watukufu wetu…basi mujitokeze mbele kwa ajili ya dhabihu hii…hivyo ningependa kuwa, kama baadhi ya vijana ambao wanatumai kukan'yaga nyayo za Hazrat Khawaja Muiin-ud-din Chishti Ajmiiri r.a. na Hazrat Shahab ud din Suharwardi r.a. Basi jinsi vijana wa Jamaati hujitolea Maisha yao kuwa Wakfu chin ya idara ya Tahrike Jadid vivyo hivyo wajitolee Maisha yao mbele yangu moja kwa moja ili niwatumie kwa namna ambavyo waweze kufanya kazi ya kuwaelimisha Waislamu. Wao waendelee kujipatia miongozo kwangu na kufanya kazi nchini. Nchi yetu haiko kame lakini iko kame kabisa kwa kiroho…kama watu wa namna hii hawatajitokeza mbele na hawatapatikana watu wa mfano wa Hazrat Muiin-ud-din Chishti, Hazrat Shahab-ud-din Suharwardi, na Hazrat Farid-ud-din wa Shakar Ganj basi nchi hii itakuwa kame zaidi kiroho….hivyo basi nataka vijana wa Jamaati waoneshe ushujaa wao na kujitolea Maisha yao kuwa Wakfu kwa lengo hili.* (*Alfazl*, 6 Feb.1958)

Hazrat khalifa tul Masih wa Pili r.a.aliwatakia Wakfiin hawa kuacha miji yao na kukaa vijiji vya mbali zaidi na kuwafundishia watu mafundisho ya Kurani Tukufu na Hadithi za Mtume s.a.w. na kuwaandaa wanafunzi wao ambao watasambaa kwenye maeneo mengine hivyo itarejea wakati ule ule uliopatikana katika enzi za Wasufia (Mawali) wa zamani. Kisha Huzur alimtaja hazrat Seyyed Ahmad wa Baraili r.a. aliyewatuma wanafunzi wake katika maeneo tofauti tofauti ya India, akiwemo Maulana Muhammad Kasim Nanotvi aliyeanzisha madrasa maarufu wa Dioband kisha Hazrat Khalifa-tul-Masih wa Pili r.a.alimtaja Hazrat Shah Wali-ullah sahib aliyeweza kuitumikia sana dini katika zama zake.

Hazrat Khalifa-tul-Masih wa Pili[ra] alisema akitoa maelezo zaidi kuhusu mpango wa Wakfe Jadid kuwa:

"Lengo langu la kuanzisha Wakf hii ni kwamba, walimu wetu wapatikane toka Peshawar hadi Karachi na katika kila sehemu kwa umbali mdogo mdogo tu yaani mwalimu wetu awepo kila baada ya kilomita kumi kumi au kumi na tano na kuendelea na madrasa… basi nawaambia marafiki wa Jamaati kuwa wajitolee jinsi wawezavyo kwa shabaha hii.(*Alfazl*,16 feb.1958)

Hazrat Musleh Al-maud[ra] alifafanua zaidi na kusema kwamba tutahitaji maelfu ya walimu ila kwa sasa tutaanza na walimu kumi lakini mpango wetu hasa ni kuanzisha vituo 1500 kwa uchache.

Mpango wa Wakfe Jadidi unajijumuisha mambo mawili ndani yake:

Wakfiin(wenye kujitolea Maisha wakfu), na mpango mzima wa malezi kuwapitia **walimu na mahubiri**

Mpango wa kujitolea mali.

Watu wengi kutoka miji mbali mbali, walijitokeza kwa ajili ya mpango huu adhimu na idadi ya Wakfiin iliweza kufika 245 ndani ya miezi miwili tu na ahadi za kutoa mchango zilizidi elfu sabini.(*Alfazl* 15 March 1958)

Kuanzishwa kwa Majlis Wakfe Jadid

Hazrat Musleh Al-Maud r.a.alianzisha mfumo wa kitanziim kwa ajili ya kusimamia shuguli zake na kuuimarisha mpango huu mpya, na Huzur aliunde "Majlis Wakfe Jadid" na kumteua bwana Munir Ahmad Bahri kuwa katibu wake na kumwambia kuwasiliana na Private Secretary wake kwa ajili ya kupata chumba kimoja katika ofici yake(private Secretary) ili ofici ya Majlis Wakfe Jadid ianzishwe pale hivyo ofici yake ya kwanza ilikuwa ndani ya ofici ya Private Secretary kisha baada ya muda fulani ilihamishwa kwenye nyumba moja ya kupanga. Hazrat Sheikh Muhammad Ahmad Mazhar aliteuliwa kuwa rais wake wa kwanza na makatibu kadhaa waliteuliwa kwa cheo cha "Nazim"na shuguli nzima ya walimu ilikuwa chini ya Nazim Irshad kisha Nizamat wa Taalim, Nizamat wa Mali na Nizamat Jaidad pia ziliundwa. Hazrat Mirza Tahir Ahmad (Aliyechaguliwa kuwa Khalifa wa Nne baadaye) alikuwa mjumbe wa Majlis toka mwanzo wake na hadi kuchaguliwa kuwa Khalifa aliendelea kutoa huduma zake katika Majlis Wakfe Jadid kama Nazim Irshad. (*Silsila Ahmadiyya* J.2.uk.551)

Wakfe Jadid nchini India:

Majlis Wakfe Jadid ilianzishwa nchini India mnamo 9 machi 1958 sawa na agizo la Khalifa-tul-Masih wa pili r.a.na Hazrat Mirza Wasim Ahmad aliteuliwa kuwa Rais wake pamoja na wajumbe 7 wengine.

Bajeti ya Kwanza:

Majlis Wakfe Jadid ilianza shuguli zake chini ya usimamizi hasa wa Khalifa wa Pili r.a. na budjeti yake ya kwanza na ya pili, yaliandaliwa katika mwezi wa January na Aprili 1958 sawa na maagizo ya Huzur kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Majlis hiyo.

Chuo cha kwanza cha Walimu:

Itaendelea toleo Lijalo

Afghanistani na chanzo cha kujikwaa

Kutoka uk. 2

kwa mtizamo wa serikali zisizo na mlengo wa Ukristo basi ipo haja kubwa kupitia na kuchunguza serikali hizo zinazodai ni za Kiislamu. Na mwishoni watabaini kuwa serekali hizo ziko mbali mno na mfumo wa serekali za Kiislamu. Kwa hakika kama serikali ya Aghanistani ingelikua ikiongozwa kwa mtazamo wa kweli wa Islamu ingeweza kuokoa maisha ya raia wengi pamoja na mali za wananchi wa taifa hilo kwa kufuata kwa uadilifu mkubwa mfumo wa utawala wa Kiislamu kwa kumuogopa Allah sawa na mafundisho ya dini tukufu ya Islamu. Hayo yanayotokea Aghanistani na nchi nyinyine zinazotawaliwa kwa mfumo wa dola za Kiislamu ni kiini macho kwa jina la vazi la Islamu, Mwandishi wa kitabu cha *Mauaji Kwa Jina la Allah* uk 137 anatetea ukweli na ubora wa dini katika kusimamia uadilifu juu ya tawala mbovu na kandamizi zinazotumia jina la dini kunyanyasa raia wake anasema *"kwamba siyo Islamu tu bali kila dini ya haki, hata ikiitwa kwa jina gani, haiwezi kuruhusu vitendo vya kikatili na kumwaga damu ya mwanaume, manamke na watoto wasio na hatia, kwa jina la Mungu"*.

Vyombo mabalimbali vya habari vya kimataifa vimeendelea kuangazia matukio kadhaa yanayoendelea kutokea na kuacha kuonyesha chanzo na mzizi wa machafuko na mahangaiko ya Waafghanistani hivi leo. Hali ya Aghanistani juu utawala wa Talibani unaipa dunia somo la kupitia upya historia ya nchi hiyo kwa makini ikiwa tunataka kupata amani ya kweli kwa kwa maslahi ya dunia juu ya hali ya kisiasa na usalama katika nchi hiyo. Historia ya Afghanistani mwanzoni ilikua ni ya kutukuka na ni nchi iliyoweza kutoa wanazuoni wengi wa fani mbalimbali ikiwamo wa dini, sharia, uchumi, sayansi nk. Kama wachunguzi wa historia watazamia kidogo tu watabaini tukio baya na bovu la kusikitisha la mauaji ya Maulana Sayyid Abdul Latif (1853 – July 14, 1903) ndio lililoitia Aghanistani katika dosari ya laana ya machafuko hadi hivi leo. Historia ndio muamuzi sahihi wa Amani ya Afghanistani kama kweli dunia inahitaji kuikomboa nchi hiyo na machafuko hayo. Maulana Sayyid Abdul Latif aliyezaliwa katika nchi ya Afganistani mwaka 1853 alikua mwanchuoni mkubwa wa dini tukufu ya Islamu na mtu maarufu katika utawala wa Amir wa Afghanistani. Alikuwa na shauku kubwa ya kufanya ibada ya Haji katika mji mtakatifu wa Makka. Aliondoka Kabul akielekea India ili kwenda katika ibada ya Hija alipofika Kadiani aliathirika sana na ukweli wa Hadharat Mirza Ghulam Ahmad[as] na akakubali kuwa mfuasi wake. Hali hii ilimfanya amkubali Hadharat Ahmad[as] kuwa ni Mtume na Imam Mahad na Masihi Aliyeahidiwa wa zama hizi. Aliporejea Afghanistani Mkuu wa dola ya Kabul Amir akatoa kibali cha kuuliwa kwa kupigwa mawe hadi kufa kama adhabu ya kuritadi kwake kwa kuacha imani hiyo ya awali na kujiunga na Ahmadiyya. Kutekelezwa kwa adhabu hiyo ya kifo cha Maulana Sayyid Abdul Latif mwaka 1903 ndio mwanzo mpya wa historia mbovu na ya kukatisha taama ya taifa la Afghanistani. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] wa Kadiani, mwanzilishi mtukufu wa jumuiya ya Ahmadiyya hakuweza kupata furaha kwa tukio hilo Mwenyezi Mungu akamjibu mahangaiko yake ya nafsi kwa kuandika akisema:-

"Na ardhi ya Kabul itaona kwamba damu hii itazaa matunda gani ya aina aina. Damu hii haitapotea bure kamwe. Hapo kabla maskini Abdur Rahman wa Jumuiya yangu aliuawa kwa dhuluma, na Mungu Alinyamaza Lakini kwa mauaji haya sasa hatanyamaza, na matokeo makubwa makubwa yatadhihirika. Basi, imesemekana kwamba marehemu shahidi alipouawa kwa kupigwa maelfu ya mawe, siku hizo hizo kipindupindu kikali kilizuka katika Kabul, na wakubwa wengi wa utawala walikufa nacho, na baadhi ya jamaa wa Amir pia waliaga dunia. Lakini hiyo siyo basi. Damu hii ilimwagwa kwa dhuluma kubwa, na katika zama hizi chini ya mbingu hautapatikana mfano wa mauaji ya namna hii. Amefanya nini huyo Amir mjinga! Amejiangamiza kwa kumwua kikatili mtu kama huyo asiye na kosa. Ee ardhi ya Kabul, uwe shahidi kwamba uhalifu mkubwa umetendwa juu yako. Ee ardhi yenye bahati mbaya, umedhalilika machoni mwa Mungu, kwani u mahali pa dhuluma hiyo kubwa" (Kitabu Tadhkiratush Shahadatain Uk. 72.)

Kwa hakika yanoyoendelea katika nchi ya Afghanistani ni zao la dhuluma hiyo niliyoieleza iliyotendwa na Amir wa Kabul na daima kama dunia haitautilia maanani ukweli wa tukio hilo na kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu basi Kabul na Afghanistani itaendelea kuwa shahidi hadi pale Mwenyezi Mungu Atakapopenda. Talibani wataendelea kuonekani ni wasaliti wa mikataba mbalimbali ya kutafuta amani ya kudumu na ugaidi utakaa kati yao mpaka pale dunia itakapotambua ukweli wa Ahmadiyya na kufuata sawasawa mafundisho ya Islam na uadilifu utakapo kuwa juu ya dhulma ndipo itakapopatikana amani ya kudumu katika taifa hilo la Afghanistani na dunia kwa ujumla.

Msikiti wa kwanza wilayani Mbarali wafunguliwa



Na Mwl Makarani Hamza Balama Mbeya

Mnamo tarehe 30-10-2021 Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya mkoani Mbeya ilifanikiwa kufanya ufunguzi rasmi wa msikiti wake katika wilaya ya Mbarali kijiji cha Ubaruku, kitongoji cha Utyego Gusa Unate ndipo hasa mahali ulipojengwa msikiti wetu.

Kwa fadhili za Allah, ufunguzi huu wa msikiti uliambatana na maadhimisho ya siku ya Siiratun – Nabi, kwa munasaba wa mwezi mtukufu wa Rabiul Awwal (mwezi wa kuzaliwa kwa Mtume Mtukufu s.a.w.) hivyo, katika siku hii kulikuwa na baraka kubwa sana ya kufanyika mambo mawili kwa wakati mmoja, yaani ufunguzi wa msikiti na Siiratun – Nabii s.a.w. (mkutano wa kukumbushana juu ya sera, tabia na khulka njema sana za Mtume Muhammad amani, rehema, baraka na salamu za Mungu ziwe juu yake daima dwamu.)

Ikumbukwe kuwa tawi hili la Ubaruku lilipatikana kwa juhudi kubwa sana za kimahubiri zilizofanywa na Sheikh wa kanda Maulana Sheikh Karim ud din Shams sahib, akishirikiana kwa ukaribu kabisa na walimu wake Mwl. Saleh Ommar Mnemo na Mwl. Makarani Hamza Balama, mahubiri haya yalikuwa ni ya kambi maalum, wakati mwingine nyumba kwa nyumba na wakati mwingine tulikuwa tunaalikwa katika misikiti ya kisuni.

Hata hivyo wakati tulipofanya maadhimisho ya siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. tawini Chimala, Mwl. Saleh aliwaalika maustadhi kadhaa kutokea Ubaruku ambapo miongoni mwao alikuwepo ustadh Sabil Miraj Simba ambaye kwa sasa ndiye Mwalimu wa Jamaat Ubaruku. Ustadh huyu alipata hamasa kubwa mno ya kujiunga na jamaat, akitokea Ubaruku mara tu baada ya kusikiliza hotuba iliyotolewa na Sheikh wa kanda kumhusu Masihi aliyeahidiwa a.s. hivyo kabla ya Sheikh sahib kuondoka, ustadh huyu alijaza baiat na kuwa mwanajamaat wakati huo huko alikotoka alikuwa ni ustadh wa kisuni. Sasa aliporudi Ubaruku changamoto zikaanza kwa huyu ustadh ndipo alipoomba nguvu kutoka kwa Sheikh wa kanda, naye bila kusita alitoka na Walimu wawili na kuelekea Ubaruku kwa huyu ustadh Sabil. MaSheikh aliokuwa amewapa taarifa kuwa Sheikh wa Kanda wa Ahmadiyya anakuja mje muuliza maswali yote, walipopata tu taarifa kuwa Sheikh amekwishatoka Mbeya kuja Ubaruku wote walikimbia na kumuachia ustadh Sabil peke yake, na ndipo ustadh huyu alipozidi kujithibitisha juu ya ukweli wa jamaat.

Sheikh na Walimu walipofika Ubaruku mahubiri ya kuwafikia watu nyumba hadi nyumba yakaendelea na ndipo baadhi ya ndugu wakaanza kujiunga na jamaat na huyu ustadh, kule msikitini akafukuzwa na akazuiliwa hata kufundisha masomo ya dini katika shule za serikali kwa kuwa tu kajiunga na jamaat. Na baada ya hapo ustadh huyu akawa na jazba ya mahubiri na familia kadhaa zikajiunga na jamaat mpaka sasa Ubaruku kuna jumla ya wanajamaat wapatao 82. Jitihada kubwa za kutafuta uwanja, kufyatua tofali ni za wanajamaat wenyewe na nguvu ya kujenga msikiti imetolewa na Sheikh wa jamaat akisaidiwa na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya Maulana Tahir Mahmood Chaudhry Sahib, na katika hatua za umaliziaji nguvu kubwa imetoka kwa Sheikh sahib akishirikiana na wanajamaat kutoka Mbeya mjini.

Sherehe za mambo yote haya mawili zilianza mnamo saa 7:30 adhuhuri mara tu baada ya kuwasili Sheikh wa kanda ya nyanda za juu kusini Maulana Sheikh Karim ud din Shams Sahib ambaye anasimamia mikoa ya Mbeya, Songwe, Rukwa, na Katavi.

Mara baada ya kuwasili Sheikh wetu huyu mpendwa, zoezi la ufunguzi wa msikiti lilianza rasmi ambapo Sheikh sahib akiwa mbele ya mlango wa msikiti akifuatiwa na kundi la wanajamaat nyuma yake aliufungua msikiti wa kwanza wa Jamaati Wilayani Mbarali kwa kukata utepe, na kuwaongoza wanajamaat wote kufanya maombi ya pamoja, ambayo Sheikh sahib alitambua uwepo wa watu wengine ambao si wanajumuiya hivyo kabla ya kuanza kwa maombi alitangaza kuwa maombi yetu yatakuwa ni ya kimya na kila mtu anaruhusiwa kuomba kwa imani yake na kwa lugha yake, kwani Mola wetu anazifahamu lugha zote.

Baada ya zoezi la maombi kukamilika, watu wote waliingia ndani ya msikitini wakiongozwa na Sheikh wa kanda ambaye ndiye aliyefungua mlango wa msikiti. Baada ya watu wote kuingia msikitini, adhana ilisomwa na Mwl. Nadhiru Ramadhani Deo kisha Sheikh sahib akaongoza sala za Adhuhuri na Alasiri.

Mara baada ya sala tu, bila kuchelewa ratiba ya mkutano ilianza rasmi kwa usomaji wa Qur'an Tukufu iliyosomwa na Mwl. Nadhiru Ramadhani Deo ambapo alisoma sura 24:56. Na baada ya usomaji wa Qur'an



Tukufu ilifuatiwa na mada ya kwanza iliyohusu "khulka za Mtume Muhammad s.a.w". Mada hiyo iliwasilishwa na Mwl. Saleh Ommar Mneno wa jamaat ya Ilongo.

Baada ya hapo ilifuatia zamu ya Sheikh wa kanda ambapo yeye alikuwa na mada isemayo "shabaha ya kujengwa kwa msikiti na muhtasari wa maisha ya mtume mtukufu Muhammad s.a.w". Ambapo katika hotuba yake Sheikh sahib alianza kwa kusema "leo ni siku ambayo ardhi ya Ubaruku na Wanaubaruku wana bahati kubwa sana kwani ni siku ambayo mambo mawili yanafanyika kwa siku moja. Hivyo upendeleo huu walioupata basi wautumie vyema kwa kuhakikisha kuwa wanautendea haki kwa kuujaza yaani kufika msikitini kwa wingi wakiiga tabia Tukufu na khulka njema za Mtume Mtukufu s.aw.".

Mara baada ya kumaliza hotuba yake Sheikh sahib alifunga mkutano huu kwa maomba ya pamoja na kugawa tamtam kwa watoto wasiopungua 80, furaha ilionekana kubwa sana kwenye nyuso za watoto hawa wote kisha washiriki wote wa hafla hii walikaribishwa kwenye chakula cha pamoja kilichokuwa kimeandaliwa na wanatawi hasa wakinamama. Mwishowe Mwenyekiti wa mtaa alitoa shukrani zake juu ya ujenzi wa msikiti huu mzuri katika mtaa wake na kueleza hisia zake kuwa msikiti huu utakuwa chanzo cha kuleta amani utulivu na ustaarabu katika jamii.

Msikiti huu ulipewa jina la *"Masjid Baitul Khabiir"* na Khalifa wetu wa zama Hazrat Mirza Masroor Ahmad, Mwenyezi Mungu Amsaidie kila siku kwa roho takatifu. Amin.

Hafla hii ya ufunguzi wa msikiti ilihudhuriwa na watu 120 wakiwemo wasiowanajamaati. Watu kama 150 wanaweza kusali ndani ya msikiti huu.

Tunawaomba wasomaji wetu wote kuwa msikiti huu uwe kituo cha kueneza nuru ya kiungu na umoja wake katika na jina la jamaati lipate kutukuka mno katika mazingira yake. Amin.

Kifo Juu ya msalaba?

Hoja kumi kutoka kwenye Biblia Takatifu

Kutoka toleo lililopita

2. MKE WA PILATO AONA NJOZI

Na alipokuwa ameketi juu ya kiti cha hukumu, mkewe alimpeleka mjumbe kumwambia usiwe na neno na yule mwenye haki, kwa sababu nimeteswa mengi leo katika ndoto kwa ajili yake (Mathayo 27:19).

Njozi ya mama yule ilikuwa ya kweli na iliyokuja wakati muafaka. Iliashiria kunusurika kwa Kristo kutokana na kifo cha laana kwenye msalaba. Mwenyezi Mungu huwaokoa waja wake kwa kupitia njozi za watu wengine kama ilivyotokea kwa Yusuf alipotoa taawili juu ya njozi mbili alizoziona Farao na akaachiliwa kutoka gerezani.

Mwenyezi Mungu alitaka kumlinda Yesu dhidi ya maadui zake na ndio maana ya njozi ya mke wa Gavana wa Kirumi. Na njozi hii ilimuathiri Gavana huyu alipokuwa anatoa hukumu yake.

3. MWELEKEO WA HURUMA WA GAVANA WA KIRUMI

Itaendelea toleo Lijalo

Bustani ya Washairi

UZURI HASA

Kwa jina Lake Kahari, ndilo ninalotamka
Anijalie khairi, niweze kueleweka
Niifikishe khabari, pale panapotakika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Kitu hupata uzuri, ukawa wa kusifika
Na tena ulo dhahiri, pote pote unawaka
Hakika unaathiri, na pia hauna shaka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Kama chakula sukari, utamu inasifika
Ailaye hudhihiri, hii tamu ya hakika
Utamuwe huathiri, ulimi husisimka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Huwa hanayo habari, homa inapomshika
Kuwa ni tamu sukari, mdomoni ikifika
Moyo wake ukihiri, na mara huitapika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Mtume mwenye fakhari, Muhammadi katamka
Husuda tujihadhari, wemani tutaondoka
Sababuni kama nari, kwenye kuni ikishika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Muhamad kadhihiri, ushahidi uso shaka
Na kwa mengi matabiri, vitabu vya kablika
Vilieleza dhahiri, ni Nabii wa Rabuka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Japo Mola Kahari, Kasema ni msifika
Vitabu vimekariri, ni mkweli aso shaka
Lakini watu jeuri, tafakuri likakuka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Hoja wakatahayari, kukosa la kutamka
Wakaipanga shari, ya mauti kumfika
Ikabidi ahajiri, Madina kutoka Maka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Ndivyo alivyodhihiri, Ahmad kwa hakika
Ushahidi wa Bukhari, Muslim kadhalika
Quran yakariri, Manabii watafika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Yeye kwa kudhihiri, dini imeimarika
Bidaa zilokithiri, zenyewe zinatoweka
Ya Muhamadi athari, inabidi kung›arika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Twangalie kwa ari, husuda kuiepuka
Ndio hasa kwa dhahiri, wema wetu hufunika
Tukashindwa jua siri, Nabii aliyefika
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Tumuombe ya Kahari, Mola Aliyetukuka
Atujuze hiyo siri, ya Nabii Msifika
Na tena Atusitiri, tukubali pasi shaka
Uzuri hasa ni kitu, au wa mtazamaji?

Hassan Sango (**Jange Muqadas, kwenye karatasi**)
Dar es salaam

NENDA BUNGA NENDA

Nenda Bunga nenda Bunga, rohoni hatuna inda
Hakuna anaepinga, sisi sote tutakwenda
Hesabu imeshafunga, imetimia kalenda
Nenda Bunga nenda Bunga, sisi tupo nyuma yako

Yale uliyoyalenga, mengi umeshayatenda
Tena sio ya kijinga, Mungu anayoyapenda
Nenda huku ukiringa, kwani unazo ajenda
Nenda Bunga nenda Bunga, sisi tupo nyuma yako

Nalia mwana wa Bunga, jinsi nilivyokupenda
Chozi lanilengalenga, sasa wapi nitaenda
Moyo wanitangatanga, mwili wangu umekonda
Nenda Bunga nenda Bunga, sisi tupo nyuma yako

Kwa jina ni Issa Bunga, nimeachwa bado kinda
Baba Hassan wa Bunga, kaondoka ameenda
Nawaarifu malenga, ziwafike kila kanda
Nenda Bunga nenda Bunga, sisi tupo nyuma yako

Hizi chache nilotunga, hazifiki beti kenda
Kuandika ninafunga, huzuni inanishinda
Ajisomee Mpinga, na wote walompenda
Nenda Bunga nenda Bunga, sisi tupo nyuma yako

Issa Hassan Bunga
Kivule, DSM

Moyo wangu umefunga,, rohoni nina fundo
Mzee Hasani Bunga, sifa zake ziko lundo
Alichukia majanga,
Mola Amuweke pema, Mzee Hasani Bunga

Mzee Hasani Bunga, Mola Amuweke pema
Ni mwepesi kama unga, Jamaat hakupima
Alipita kila anga, tusiipate dhuluma
Mola amuweke pema, Mzee Hasani Bunga

Beti tatu kwa malenga, Mhariri ninalia
Ewe Musa wa Mpinga, Tawile Issa kalia
Najua unajipanga, tenzi zilizotulia
Mola Amuweke pema, Mzee Hasani Bunga

Mhariri

NAKUPENDA AHMADIYYA

1.Utukufu wa mbinguni, na ule wa ardhini.
Mmiliki ni rabani, mola rabbil ghalamin.
Aloniangaza dini, dini yake ya manani.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

2.Muhammad lake jina, la pili umechukua,
Ahmadi ndio jina, kwake ulilolitwaa.
Kuongoza insana, ili wasije potea.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

3.Umetokea jangwani, barani uarabuni.
Kwa mafundisho ya dini, yaliyo jaa amani.
Ukashinda nafsi duni, islam ikawa ndani.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

4. Elfu moja nne mia, miaka ilipofika.
Dunia alitujia, tulomngoja kufika.
Seyyidna Ahmadiyya, kujaeleza hakika.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

5. Rahmani limwambia, apande mbengu ya insa.
Ahmadiyya ikanzia, moja nane nane tisa.
Na giza kuliondoa, dini ya kufwata visa.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

6.Mungu mmoja twaomba, bila ya kushirikisha,
Uvivu hujatukumba, wa mola kumdumisha.
Kwa sauti twajigamba, hata kitukufurisha.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

7. Quran kisha na sunnah, hadithi zinafwatia.
Ndiyo tunavyojivuna, mwongozo wa kushikia.
Maneno ya kujashona, mbali twayatupilia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

8. Tunachopata hutoa, dini kuindeleza,
Mbinguni kujijengea, majengo ya kupendeza.
Kilicho bora achia, kwa Mungu Mola muweza
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

9.Sala tano kila siku, kwa kudumu simamisha .
Tahajudi za usiku, nazo kuzihimarisha.
Tunaomba kwa shaukiu, al mujibu pitisha.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

10. Al qayyum wa milele, pekee atabakia.
Viumbe vyote vifile, nuruye itabakia.
Ni yule yule wa kale, ametudhihirikia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

11. Kwa ishara kuonesha, kwetu si hutuletea.
Matetemeko hushusha, kwa wanaotukataa.
Kwetu sisi mepusha, balaa kutotutia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

12. Rahiim hajatuacha , kila mtu kuamua.
Katuchgulia picha , khalifa wa mfanoa.
Bila ya kushika ncha, amani kuhubiria.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

13. Kiongozi wa mfano, dunia kuionyesha.
Suluhu na maungano, dunia kuifundisha.
Kuondoa migongano, islam yafundisha.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

14. Mapenzi yetu kwa wote , bila chuki kwa yeyote.
Kauli mbiu ya wote, upendo pande zote.
Bila tazama chochote, kwa waabudu chochote.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

15. Twasema hayo kwa moyo, pia kwa kudhihirisha.
Rehema iso na choyo, islam yafundisha.
Na huruma ya mioyo, daima tunadumisha.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu.

16. Nimejaribu tafuta, wala kasoro sioni.
Kwa ukweli wa kuvuta, uliojaa yakini.
Ya mola kumtafuta, yajiweka hadharani.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

17.Mafunzo ya qurani, hadharani kuyaweka.
Toka lile la mwanzoni, hadi la mwisho kushuka.
Nayo elimu ya ndani, kwa watu kuipeleka.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

18. Tayari kuweka kando, ya uzushi walotia.
Pia kufungua pindo, ya manani kukazia.
Ni washetani upindo, akili kuiachia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

19. Kama sifa za kusifu, ni hiii yaifalia.
Yaepuka upotofu, wa mambo kujitungia.
Ile ya zama nyoofu, imani twaifatia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

20. Nimejaribu kusema, machache yalonijia.
Naombeni kusimama, na kalamu kuachia.
Kwa uwezo wa karima, kwa hapa lipofikia.
Nakupenda Ahmadiyya, mwanga wa maisha yangu

Masihi Omary Stambuli (**KISAGWA**)

JIUNGENI NAMI

Mie jua la Baraka, Sayari nizungukeni
Na kwenu sina Mipaka, Mpatapo nizuruni
Na msipo bahatika, Kwa barua sabahini
Kwa waso elimika, Niwekeni sujudani
Ni sauti iitayo, Upande wa Ukhalifa

Shunda Mshudia wana
Daluni, Tanga

KUYAKUMBUKA SIWEZI

Muhali kuyakumbuka, makosa niliyotenda
Ila umeyaandika, ya heri na yenye inda
Ninakuomba Rabuka, nyoosha palipopinda
Wewe Shadid likabu, ila pia husamehe

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani, Migombani, Dar es salaam

HOFU YETU MOLA WETU

Dunia yote gizani, Zimefugwa njia zote
Mawazo karantini, Hofu ipo pote pote
Ulimwengu hatarini,Kufutika tuokote
Wewe ndio kimbilio, Mola wetu tunusuru

Janga juu ya majanga, Ila hili ni Kisanga
Wenye mitaji ya kanga, Machinga kutangatanga
Hakuna pa kuzichanga, Huu wa shingo upanga
Masharti tunafwata, Mola wetu tunusuru

Tumrejeeni Karima, Na dua ndo suluhisho
Amimine takrima, Atukinge na vitisho
Tii Khalifa wa zama, Hili langu hitimisho
Hofu yetu Mola wetu, Mengineyo yakupita

Shabani A. Shunda
Shunda Mshundia Wana
Daluni Tanga

Viazi, Mayai na Buni

Hapo zamani za kale binti mmoja alimlalamikia baba yake kuwa maisha yake yalikuwa magumu na hajui atafanyaje. Alikuwa amechoka kupambana na kuhangaika kila wakati. Ilionekana kama tatizo moja likitatuliwa, lingine linafuata upesi.

Baba yake, mpishi, alimpeleka jikoni. Alijaza sufuria tatu za maji na kuweka kila moja kwenye moto mkali. Mara tu sufuria tatu zilipoanza kuchemka, aliweka viazi kwenye sufuria moja, mayai kwenye sufuria ya pili na buni ya kusaga kwenye sufuria ya tatu. Kisha akaacha vichemke bila kusema neno na binti yake. Binti alilalama na kungoja bila subira akijiuliza anafanya nini. Baada ya dakika ishirini alizima majiko. Alitoa viazi kwenye sufuria na kuviweka kwenye bakuli. Akatoa mayai na kuyaweka kwenye bakuli. Kisha akaiweka kahawa na kuiweka kwenye kikombe.

Akamgeukia, akauliza. 'Unaona nini?' "Viazi, mayai na kahawa," alijibu kwa haraka.

"Angalia kwa karibu," alisema, "na uguse viazi." Alifanya hivyo na akabainisha kuwa vilikuwa laini.

Kisha akamwomba achukue yai na kulivunja. Baada ya kung'oa ganda, aliona yai lililochemshwa.

Hatimaye, alimwomba anywe kahawa. Harufu yake nzuri ilileta tabasamu usoni mwake.

"Baba, hii inamaanisha nini?" Aliuliza.

Alieleza kuwa viazi, mayai na buni vimekabiliwa na shida sawa - maji yanayochemka. Hata hivyo, kila kimoja kiliitikia tofauti.

Viazi viliingia viguvu, ugumu usio na nguvu, lakini katika maji ya moto, vikawa laini na dhaifu. Yai lilikuwa tete, huku ganda jembamba la nje likilinda maji yake ya ndani hadi lilipowekwa kwenye maji yanayochemka. Kisha ndani ya yai kukawa kugumu. Hata hivyo, buni ilikuwa ya kipekee. Baada ya kufunuliwa na maji yanayochemka, ilibadilisha maji na kuunda kitu kipya.

TAFUTA MANENO

Yatafute maneno 25+ hapo chini kwa kuyazungushia na Penseli

U	S	H	I	R	I	K	I	A	N	O	J	F	A	X	E	Y	G
D	M	M	K	T	A	H	R	I	K		L	H	T	B	Y	I	T
M	G	A	U	S	H	I	R	I	K	A	S	V	A	X	Z	D	J
M	V	U	C	P	X	K	H	P	T	A	K	B	F	U	M	C	Y
A	L	U	N	N	M	M	Z	M	R	N	U	D	G	N	A	J	B
L	B	D	N	M	D	R	W	B	A	U	V	A	X	F	J	A	B
E	U		G	A	L	H	A	A	F	S	B	N	T	H	A	M	M
Z	K	J	L	L	L	K	U	I	L	U	I	W	B	M	R	A	N
I	H	A	R	I	R	M	R	L	A	I	N	H		T	I	A	V
R	A	G	H	P	D	I	R	B	U	K	M	A	I	K	B	T	T
C	R	Q	M	M	H	I	I	R	U	M	N	U	B		U		T
L	I	C	L	D	A	T	N	M	N	A	A	N		L	C	T	M
R		J	A	T	A	D	E	I	L	F	A	L	S	A	F	A	
G	T	B	V	K	D	H	I	U	H	P	Q	G	T	R	Y	G	P
R	U	D	H	J	E	U	A	Y	J	G	T	M	A	I	T	I	
V	P	K	T	R	G	M	N	F	Y	M	L	J	K	R	L	R	W
N	K	Y	A	J	P	M	C	I	N	A	B	U	S	H	A	R	I
R	P	M	B	D	J	T	K	L	A	M		K	W	G	F	L	G

UNGANISHA NUKTA

Unganisha nukta ili upate picha moja iliyokamilika.



Jinsi ya kupika Donat

Na **Mtandao**



MAHITAJI
1. Unga wa ngano kilo 1
2. Mafuta ya kupikia lita 1
3. Sukari ilosagwa robo kilo
4. Hamira
5. Siagi
6. Maziwa robo lita
7. Mdalasini ulosagwa
8. Mayai 3
9. Baking powder kijiko 1 kikubwa

Namna ya kupika donat

1. Changanya unga na baking powder pamoja na siagi hadi unga uchanganyike tia sukari kidogo, kungumanga na yai kisha endelea kuchanganya unga.
2. Weka maziwa na kanda mpaka upate donge laini tengeneza madonge, uanze kusukuma unga kiasi cha sentimeta moja. Usiwe mwembamba sana kama wa chapati.
3. Kata duara kwa glasi au kikombe kisha kata duara lingine dogo katikati kwa kutumia kifuniko cha chupa ya maji au kitu chochote chenye duara dogo, upate shepu ya ringi.
4. Bandika mafuta jikoni, yakipata moto tia donats uzikaange mpaka ziwe na rangi nzuri ndipo uzitoe.

بسم الله الرحمن الرحيم

AHMADIYYA SECONDARY SCHOOL - KITONGA

Registration No. S 4681 **Centre No. S.5081**

P. O. Box 376, Dar es salaam. Tel: 2110473, Fax 2121744 Email: ahmadseckitz@hotmail.com

Shule ya Sekondari Ahmadiyya inakutangazia nafasi za kujiunga na kidato cha kwanza 2022. Shule ni ya wasichana na wavulana, ipo Kitonga kata ya Msongola Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam.

Ada zetu ni: **Tsh 1,200,000/= kwa wanafunzi wa bweni**
Tsh 700,000/= kwa wanafunzi wa kutwa

ambayo hulipwa kwa awamu nne.

Pia shule ina nafasi ya kuhamia wanafunzi.

Ofa zitolewazo ni pamoja na;

✳ Ufadhili wa ada kwa mwanafunzi anayefaulu vizuri.

Mawasiliano:

0713 055 898 (Mkuu wa shule)

0787 579 735 (Meneja wa shule)

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

Kurudisha Kiumbe

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

إِلَيْهِ مَرْجِعُكُمْ جَمِيعًا ۖ وَعْدَ اللَّهِ حَقًّا ۚ إِنَّهُ يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ لِيَجْزِيَ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ بِالْقِسْطِ ۚ وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ شَرَابٌ مِنْ حَمِيمٍ وَعَذَابٌ أَلِيمٌ بِمَا كَانُوا يَكْفُرُونَ)

Surat Yunus 10: 5

Kwake ndiyo marejeo yenu nyote. Ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli. Hakika Yeye ndiye huanzisha kiumbe kisha Hukirudisha ili Awalipe walioamini na kufanya vitendo vizuri kwa adili. Lakini waliokufuru, wao watapata kinywaji cha maji yachemkayo na adhabu iumizayo kwa sababu walikuwa wakikataa.

KURUDISHA KIUMBE kunakotajwa hapa kunahusu, 1. kwanza, baada ya kufa mwanadamu atapewa uhai mpya, na katika uhai huo matendo yake aliyofanya hapa duniani yatalipwa; na 2. pili, hata katika dunia hii vizazi vya wanadamu vinaandamana ili matendo mema ya kizazi kilichotakadamu (kilichotangulia) yasipotee bure na yawafae watu wa kizazi kinachowaandamia.

Mola wetu! Utupe katika wake zetu na watoto wetu yaburudishayo macho, na Utujaalie kuwa viongozi kwa wamchao (Mungu). Amin

NUKUU YA HADITHI

Na **Ustadhi Issa Malenge** - 0625 914 740 0752 334 332

حدثنا عفان حدثنا أبو خلف موسى بن خلف كان يعد في البدلاء حدثنا يحيى بن أبي كثير عن زيد بن سلام عن جده ممطور عن الحارث الأشعري أن نبي الله صلى الله عليه وسلم قال إن الله عز وجل أمر يحيى بن زكريا عليهما السلام بخمس كلمات ..... وأنا آمركم بخمس الله أمرني بهن بالجماعة والسمع والطاعة والهجرة والجهاد في سبيل الله فإنه من خرج من الجماعة قيد شبر فقد خلع ربقة الإسلام من عنقه إلا أن يرجع ومن دعا بدعوى الجاهلية فهو من جثاء جهنم قالوا يا رسول الله وإن صام وإن صلى قال وإن صام وإن صلى وزعم أنه مسلم فادعوا المسلمين بأسمائهم بما سماهم الله عز وجل المسلمين المؤمنين عباد الله عز وجل. (مسند أحمد بن حنبل)

Imesimuliwa na Hadhrat Harith Ash'ar r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema:
Hakika Allah alimuamrisha Yahya bin Zakariya mambo matano .....
Nami nawaamrisheni matano ambayo Allah ameniamrisha ,
Nayo ni haya :

- Kaeni katika Jamaat (Jumuiyya).
- Sikilizeni sana (Maneno ya Amir)
- Tiini mnayoamrishwa .
- Kuhama (makaazi yako kama kuna haja ya dini)
- Kupigana Jihadi katika njia ya Allah.

Kwani aliyetengana na Jumuiyya sawa na shibiri ameachana na Islaam isipokuwa arejee tena .
Na yule anayeita kwenye mambo ya ujahili (ya kabla ya Islaam) ndiye kuni ya Jahannamu.
Wakauliza : Hata akifunga swaumu na akisali , Ewe Mjumbe wa Allah ?.
Akajibu : Naam, hata akifunga na akisali na kujidhania kuwa Mwislaam!.
Na hata hivyo waiteni waislaamu wanaojiita waislaam,
Kwani Allah mtukufu amewaita waislaam, waaminio, watumishi wa Allah Subhana wata'ala.
(Musnad Ahmad).

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA as

Amri za Huruma

Nimejulishwa ya kwamba miongoni mwa Manabii wote, yule aliyefikisha mafundisho matimilifu na safi yaliyojaa busara na yule aliyeonyesha nafsini mwake khulka bora zaidi za kiutu ndiye Mtume Mtukufu Muhammad, Bwana na Kiongozi wetu, amani na baraka za Mungu ziwe juu yake.
(Roohani Khazain Jal. 17: Arbaeen No.1 Uk. 3)

MATUKIO KATIKA PICHA





Hafla ya ufunguzi wa Siku za michezo katika chuo chetu cha Kidini Jamia Ahmadiyya Tanzania Mheshimiwa Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiyaya Waislamu Waahmadiyya Tanzania alifungua rasmi na Maombi. Mwenyezi Mungu Awabariki washiriki wote. Amin











Tabligh & Tarbiyyat Visit to Zanzibar

Mheshimiwa Sh Tahir Mahmood Chaudhary Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania alitembelea wanajumuiya na viongozi wa kamati mbalimbali katika Zanzibar.





Khalifa Mtukufu atoa hotuba ya kusisimua imani akifunga Ijtimaa ya Khuddam Uingereza

Kutoka uk. 11

maneno haya kama tathmini kwao kwa maisha waliyoishi, ambapo wanapaswa kuyaingiza katika majukumu yao ya kuimarisha taifa lao kwa kujiimarisha wao wenyewe. Hivyo basi, mnapaswa kufanya juhudi ili kufikia kiwango cha juu kabisa cha maadili na kiimani na kuwa wa thamani zaidi kwa taifa lenu na Jumuiya, ama sivyo kuyarudia tu maneno haya bila vitendo ni jambo lisilo na maana kabisa."

Khalifa Mtukufu^{atba} pia alialezea kwamba ili mtu aweze kuhudumia na kujitolea kwa ajili ya '**Imani yake, nchi na taifa lake**' kama wanachama wa Khuddamul Ahmadiyya wanavyosema katika kiapo chao, kitu cha kwanza cha lazima katika vitendo vyao ni kutekeleza sala tano kila siku.

Akifafanua kuhusiana na namna gani mtu anaweza kutekeleza ibada ya sala, Khalifa Mtukufu^{atba} alisema:

"***Lazima utekeleze ibada ya sala tano kila siku. Na sio haraka haraka bila ya kuwa na mazingatio. Bali sala yako inatakiwa kutekelezwa kwa umakini, na mazingatio makubwa na mapenzi ya kweli ya Allah yawe ndani ya moyo wako.***"

Khalifa Mtukufu^{atba} aliendelea kusema:

"***Tumia muda huo wa wakati wa sala kujenga uhusiano wako na Allah na usifanye maombi tu kwa ajili yako na familia yako bali pia uombe kwa ajili ya Imani yako, Jumuiya na taifa lako.***"

Pia Khalifa Mtukufu^{atba} alitoa ushauri wa vitendo wa namna gani watu wanaweza kujiimarisha wenyewe.

Khalifa Mtukufu^{atba} alisema:

"***Endapo kila mwezi, utafanya juhudi thabiti ya kuacha jambo moja baya, huku ukijitahidi kutwaa tabia moja njema au wema mmoja uliyofundishwa na Qur an Tukufu, kisha ndani ya mwaka mmoja, utafanikiwa kuokolewa kutoka katika makosa mengi na yatafidiwa na vitendo vingi vyema. Jinsi unavyozidi kutembea katika njia ya wema na haki, ndivyo unavyozidi kupata wema na kuuondoa uovu kwasababu wema huzaa wema na uovu huzaa uovu.***"

Akitaja kwa umaalum viwango vya ukweli, Khalifa Mtukufu^{atba} alirejea maneno ya Masihi Aliyeahidiwa^{as} kuhusiana na hili:

"***Mtu anapaswa kuachilia mbali aina zote za ushirikina na uongo. Kwa kweli, uongo pia ni ushirikina na yeyote atakaejiegemeza katika hilo basi ni yeye ndie anayeachana na ukweli wa Allah. Hivyo, kwa kusema uongo mtu anaachana na Allah.***"

Khalifa Mtukufu^{atba} pia alitaja umuhimu wa kuwa mwema, mwenye huruma na kuwajali watu wengine.

Khalifa Mtukufu^{atba} alisema:

"***Kwa taifa au jamii kuwa imara inahitajika watu wake kuungana pamoja na kujaliana kila mmoja na kushirikiana kila moja katika furaha na huzuni. Inasikitisha, wakati mwengine vitu vidogo sana visivyo na maana au ugomvi usio na maana unatokea na kusababisha matatizo makubwa na hata kupigana miongoni mwa watu wanaopaswa kuwa kama ndugu.***"

Khalifa Mtukufu^{atba} aliendelea kusema:

"***Hivyo, mara zote tendeane kila moja wenu kwa mapenzi na huba na tafuteni kutengeneza maelewano ya kweli miongoni mwenu… Endapo tunataka kuwa chini ya kivuli cha Rehema na Neema za Allah, lazima tuonyeshane mapenzi kwa kila mmoja wetu. Tunapaswa kuweka pembeni chuki zote na kuwa na mapenzi na kusameheana. Hivi ndivyo tutakavyoweza kutengeneza mahusiano ya kweli yenye mapenzi na maelewano ili kupata mapenzi ya Allah Mwenye Enzi.***"

Khalifa Mtukufu^{atba} pia alisema kuhusiana na umuhimu wa wanachama ambao wanasoma, kuzingatia kwa umakini masomo yao na kuzidi kutafuta elimu katika kada yoyote wanayoitaka.



Khalifa Mtukufu^{atba} alisema:

"***Wanafunzi wote, wa umri wowote au daraja lolote, wanapaswa kufanya juhudi na kutafuta matokeo mazuri, na jinsi unavyokuwa mtu mzima ndivyo unavyopaswa kufikia daraja la juu la utaalamu wako. Hasa vijana wetu wa Kiahmadiyya lazima watafute kujiunga na taaluma nzuri au kazi nzuri, iwe serikalini au sehemu nyingine yoyote na kufikia daraja la juu.***"

Khalifa Mtukufu^{atba} aliendelea kusema:

"***Isiwe kwa Khuddam wetu kuacha elimu mara baada ya kufikia kiwango cha sekondari na kuanza harakati za kutafuta hela rahisi, bali wanapaswa kundelea na elimu ya juu na kupata viwango bora vya elimu.***"

Akiwahamasisha wanachama wa Khuddam ili waweze kupambana zaidi katika hili, Khalifa Mtukufu^{atba} alitoa changamoto kwa wanachama wa kiume wa Jumuiya.

Khalifa Mtukufu^{atba} alisema:

"***Hivi karibuni, imedhihirika katika Jumuiya yetu kuwa vijana wa kike wamekuwa bora zaidi katika elimu kuliko vijana wa kiume. Kuhusiana na hili, naomba niwape changamoto wanachama wa Majlis Khuddamul Ahmadiyya kupambana ili kuondoa utofauti huu na kufanikiwa kufikia mafanikio makubwa ya kielimu katika kazi zenu.***"

Khalifa Mtukufu^{atba} aliendelea kusema:

"***Endapo mtafanikiwa, haitakuwa mafanikio yenu pekee bali pia itawanufaisha jamii nzima na itakuwa njia ya kuonafahari kwa Jumuiya yetu na kuendelea kupata hadhi na heshima. Mafanikio yenu pia yanaweza kutuhakikishia mafanikio ya kielimu ya kizazi chetu kijacho InshaAllah, ambacho kitajifunza kutoka kwenu. Kwa namna hii, mafanikio yasiyokuwa na kikomo ya kielimu, yataendelea kuzalika ndani ya vijana wetu InshaAllah.***"

Akihitimisha Khalifa Mtukufu^{atba} aliomba:

"***Allah awajaalie nyote uwezo utakaowawezesha kutimiza wajibu wenu na majukumu yenu kama wanachama wa Majlis Khuddamul Ahmadiyya. Awawezeshe kutimiza haki za Allah na viumbe wake na muwe wale wenye kuangaza vyema jina la Jumuiya yetu duniani kote na kutekeleza majukumu mahsusi yanayopelekea kutimiza kwa lengo kuu la Masihi Aliyeahidiwa^{as}. Ni matumaini yangu na maombi yangu kuwa mmefanikiwa katika hili. Allah mwenye Enzi aendelee kuwabariki Majlis Khuddamul Ahmadiyya katika nyanja zote. Amin.***"

Baada ya khotuba yake Khalifa Mtukufu^{atba} alizindua aina mpya ya tovuti inayoitwa '**Salat Hub**', ambayo imetengenezwa kwa ajili ya kujifunza sala katika namna iliyo shirikishi.

Ijtimaa ilihitimishwa kwa maombi ya kimya kimya yaliyoongozwa na Khalifa Mtukufu^{atba}.

Khalifa Mtukufu atoa hotuba ya kusisimua imani akifunga Ijtimaa ya Khuddam Uingereza

Kutoka uk. 12

kusema:

"Mkutano wa Ijtimaa unakupa nafasi ya kujiweka mbali na matamanio ya kidunia na kuelekeza muda wako na nguvu yako katika kujifunza na kupata uzoefu kutoka katika Khotuba zinazotolewa, mashindano na kazi mbalimbali ambazo zitakuza Uchamungu na kiwango chako cha imani."

Khalifa Mtukufu[atba] alieleza lengo jengine kuu la Ijtimaa (Mikutano) ya Tanzeem zote za Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya ni kuhakikisha kwamba kila mmoja anakuwa katika nafasi yake na anatambua malengo na thamani yake katika Jumuiya.

Kuhusiana na hili, Khalifa Mtukufu[atba] alisema:

"Kila tanzeem inafanya Ijtimaa yao ili kuwakuza kiimani wanachama wao kupitia kazi mbalimbali ambazo zinafanywa na wao wenyewe kutegemeana na umri na uelewa wao… Wanajadiliana kwa pamoja changamoto mabalimbali zinazowakabili na mambo mabalimbali yanayowakabili wanachama wao kwa kila tanzeem na namna ya kutatua changamoto hizo kiasi ambacho watataweza kutimiza amri za Allah Mtukufu katika namna iliyo bora."

Khalifa Mtukufu[atba] aliendelea kusema:

"Zaidi ya hayo, Ijtimaa zinafanywa ili kuhakikisha kwamba kila Ahmadiyya mwanamme kwa mwanamke na bila kuzingatia umri wao, makabila yao, historia zao, wanaelewa kuwa wao ni watu wenye thamani kubwa na umuhimu mkubwa katika Jamaat…Hasa Khuddam na Atfal wote wanatakiwa watambue kuwa wao wanathamani kubwa na kwamba kila Ahmadiyya ni mwenye thamani kubwa katika Jumuiya hii ya Masihi Aliyeahidiwa[as]."

Baada ya kuelezea thamani isiyo ya kifani ya kila mmoja wetu katika Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Khalifa Mtukufu[atba] alisisitiza umuhimu wa thamani hiyo vile vile uweze kuonekana na kuthibitishwa.

Khalifa Mtukufu[atba] alisema:

"Thamani hii isichukuliwe kwa urahisi (isichukuliwe poa), bali inaweza kubaki thabiti na kukubalika endapo tu mtatambua kuwa kila mmoja wenu ana jukumu la kufanya katika kudumisha hadhi ya Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa[as] na kuhakikisha kwamba inapata maendeleo na ustawi."

Akizungumza kuhusiana hasa na jukumu muhimu ambalo kijana anapaswa kulifanya Khalifa Mtukufu[atba] alisema:

"Kimsingi watoto na vijana wa taifa lolote wana jukumu kubwa la kufanya katika maendeleo na ustawi wa jamii yao. Hasa, jamii ambayo watoto na vijana wake wameingizwa katika mwamko wa kuhudumia na kujitolea katika Imani yao na ndio hao ambao wamepangiwa kufikia kiwango cha juu cha mafanikio na maendeleo."



Wakati akihutubia, Huzuur[atba] pia alizungumza kuhusiana na umuhimu wa Tanzeem zote kufanya kazi kwa pamoja.

Akielezea jukumu hili kwa kina, zaidi ya wafanyakazi na viongozi, Huzuur alisema:

"Kila mwanajumuiya, hata ambao sio viongozi, daima wanapaswa kutambua kuwa wana jukumu binafsi katika kutimiza malengo ya Masihi Aliyeahidiwa[as]. Kila mmoja wenu ameweka ahadi (Kiapo cha utii) kwa Masihi Aliyeahidiwa[as] na kuahidi kwamba daima atatanguliza Imani yake na dini dhidi ya vitu vyote vya kidunia. Ahadi hizi pekee hazina maana na zitakuwa na maana endapo tu mtafanya juhudi kuhakikisha kuwa mnazitekeleza kwa vitendo."

Huzuur aliendelea kusema:

"Mnapaswa kujielekeza zaidi katika jukumu kuu la Jumuiya, ambalo ni kueneza ujumbe wa Islam katika kila kona ya dunia hii na kueneza mafundisho ya Qur an Tukufu na Mtukufu Mtume saw na wakawa watiifu kabisa kwa Ukhalifa wa Zama basi kiwango cha maendeleo ya Jumuiya yetu kitaongezeka maradufu."

Khalifa Mtukufu pia alisisitiza juu ya umuhimu wa wanachama wa Majlis Khuddamul Ahmadiyya kutambua jukumu lao la muhimu la kukuza kizazi kijacho.

Huzuur[atba] alisema:

"Wengi wenu mmebarikiwa kupata watoto na sasa mnajukumu la moja kwa moja kwa kizazi kijacho cha Jumuiyya yetu…Ukweli ni kwamba jukumu na thamani ya baba inaelezwa na Hadithi ya Mtukufu Mtume saw kwamba hakuna zawadi kubwa ambayo baba ametoa kwa watoto wake zaidi ya kuwapatia adabu njema… Endapo umedhamiria kabisa kuwaachia watoto wako Zawadi bora kabisa, basi lazima kwanza ujiangalie mwenyewe na kuhakikisha kwamba unatekeleza wema na kwamba ni mfano wa kuigwa kwa watoto wako."

Khalifa Mtukufu[atba] aliendelea kusema:

"Msifikirie kwamba tabia zenu au vitendo vyenu havina athari yoyote kwa watu wengine. Bali, kizazi kijacho kinawaangalia moja kwa moja kwenu na kwa maanahiyobasimsiwaangushe… Endapo watakwenda kinyume, basi mtawajibika."

Akiwakumbusha wanachama wote wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kuhusiana na bidii na neema zinazotakiwa kufanywa ili kuonyesha mfano Mwema katika dunia, Khalifa Mtukufu[atba] alisema:

"Daima kumbukeni kuwa sisi ni Jumuiya ya watu ambao wamemkubali Imam wa Zama, Masihi Aliyeahidiwa[as] ambaye aliahidi kwamba tutaeneza mafundisho sahihi ya Mtume Mtukufu saw mpaka katika kila kona ya dunia hii… Hivyo basi, hatupaswi kupumzika mpaka tuwe na uhakika kuwa kila mwanajumuiya hataacha juhudi yoyote katika kuhakikisha kuwa anapata ukaribu na Allah Mtukufu."

Khalifa Mtukufu[atba] aliendelea kusema:

"Kama vile jua linavyoendelea kuchomoza kila siku asubuhi bila kushindwa, nasi kila siku yetu inapaswa kuamsha habari njema za maendeleo ya kiroho na maendeleo ya wanajamaat… Mpaka tufikie hali hiyo, ama sivyo hatuwezi kuridhika."

Khalifa Mtukufu[atba] pia alisema kuhusiana na umuhimu, na maadili ya kauli mbiu ya Majlis Khuddamul Ahmadiyya ambayo imetolewa na Khalifa wa pili wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya[rh]

Khalifa Mtukufu[atba] alisema:

"Katika mabango yenu, kwa fahari kabisa mmeiandika kauli mbiu hiyo ya Khuddamul Ahmadiyya iliyotolewa na Hazrat Musleh Maud r.h kwamba 'Taifa lolote haliwezi kuimarika bila kuimarisha vijana wake… Hata hivyo, haya sio tu maneno au kauli mbiu ya kujifagharisha nayo bali iwaamshe wanachama wa Khuddamul Ahmadiyya na kuwahamasisha."

Khalifa Mtukufu[atba] aliendelea kusema:

"Kauli mbiu hii imewekwa hapa kwa makusudi katika shughuli yenu hii ili maneno haya mazito yawaingie mioyoni mwenu na katika akili ya kila Khuddam. Hasa, kila Khuddam, wawe viongozi au wasiwe kiongozi, wanapaswa kuyachukulia

Endelea uk 10

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SAFAR - JAM.I 1443 AH | OKT - DIS 2021 | TAB.-FAT 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu[saw]

Imesimuliwa na hadhrat Ibn Umar[ra] ya kuwa: Mtume[saw] alisema: "Msijihusishe katika mazungumzo mengi isipokuwa yanayohusika na kumkumbuka Allah. Maana kuzungumza sana bila ya kumtaja Allah huufanya moyo kuwa mgumu! Na mtu aliye mbali sana na Allah ni mwenye moyo mgumu" (**Tirmidh**)

Khalifa Mtukufu atoa hotuba ya kusisimua imani akifunga Ijtimaa ya Khuddam Uingereza



"Kama Jua linavyochomoza kila siku asubuhi bila kushindwa, na sisi kila siku yetu inapaswa kuleta maendeleo na mabadiliko chanya ya kiimani kwa kila mwana Jumuiyya hii" – Hazrat Mirza Masroor Ahmad

Mnamo tarehe 19 Septemba 2021, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Duniani, Khalifa Mtukufu wa tano, Hazrat Mirza Masroor Ahmad[atba] alitoa khotuba ya kusisimua kiimani wakati wa kufunga Ijtimaa ya kitaifa (Mkutano wa mwaka) wa Umoja wa vijana wa Kiahmadiyya Uingereza (Majlis Khuddamul Ahmadiyya).

Mkutano huu wa siku mbili (2) ulifanyika katika eneo la Old Park Farm mjini Kingsley ambapo Zaidi ya Khuddam na Atfal 3,200 wenye umri kati ya miaka 12 na 40 walifanikiwa kushiriki kutoka sehemu mbalimbali za Uingereza. Mada kuu ya ijtimaa ya mwaka huu ilikuwa ni "**Nguvu ya Durood**"- kumsalia Mtume Mtukufu Muhammad (Rehema na Amani ziwe juu yake).

Wakati wa kutoa khotuba ya kufunga mkutano huu Khalifa Mtukufu[atba] aliongea kuhusu madhumuni makubwa ya Ijtimaa na umuhimu wa kuelewa moyo wa kujitolea katika kazi na majukumu.

Akiangazia katika lengo kuu la mikusanyiko ya kidini, kama Ijtimaa, Khalifa Mtukufu[atba] alisema:

"Ni muhimu sana kutambua lengo kuu la Ijtimaa sio kwa ajili ya Khuddam na Atfal kukutana pamoja na kufurahia kukutana kwao. Bali lengo la kweli na lengo kuu la Ijtimaa ni la kupata maendeleo ya kiroho, kimalezi na kiimani kwa washiriki."

Khalifa Mtukufu[atba] aliendelea

Endelea uk 11

KITABU



Serekali ya Kiingereza na Jihadi

Jihad ni nini na kwa nini Islamu ililazimika kuamua kujilinda katika historia yake ya mwanzo?

Kwa nini fikra potofu kuhusu jihad zimekita mizizi katika akili za baadhi ya makundi ya Kiislamu na ni sehemu gani ambayo viongozi wa dini ya Kiislamu na makasisi wa Kikristo wamechukua katika mchakato huu?

Je, ni halali kwa Muislamu kuasi dhidi ya serikali inayodumisha sheria na amani na kuruhusu uhuru wa dini?

Maswali haya, ambayo yamekuwa yakitupiwa macho ulimwenguni pote leo, yalijibiwa zaidi ya miaka mia moja iliyopita kwa mwongozo na uelewa toka kwa Mungu na mtu aliyedai kuwa Masihi Aliyeahidiwa.

Jipatie nakala yako kwa bei ya maktaba ya Tsh· 2,800/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com